

# HABARILEO

Jumamosi



## MAZISHI YA SUMARI

Chadema imehamishia Dar mkutano wake wa Kamati Kuu kutoka Zanzibar, ili ishiriki kikamilifu mazishi ya Sumari.

UK 2

## TORRES NA DROGBA

Andre Villas-Boas amesisitiza kuwa Torres hana tatizo akilini kuhusu Drogba kama Ancelotti anavyodhani.

UK 30

GWIFI LA HABARI TANZANIA

ISSN 1821-570X TOLEO NA. 01857 JUMAMOSI JANUARI 21, 2012 TSH. 500 KSH. 50

TANZANIA

# Chadema yahamisha kikao kumlilia Sumari

Na Waandishi Wetu, Arusha

**C**HAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimelezimika kuhamishia mkutano wake Dar es Salaam wa Kamati Kuu uliokuwa ufanyike Zanzibar, ili wajumbe wake waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za mazishi za Mbunge wa Arumeru Mashariki, Jeremiah Sumari.

Sumari aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana na baadaye Naibu Waziri wa Fedha katika awamu ya kwanza ya utawala wa Rais Kikwete, alifariki dunia juzi jijini Dar es Salaam baada ya kusumbuliwa kwa muda mrefu na maradhi ya saratani ya ubongo. Atazikwa keshokutwa Jumatatu

kijijini kwake Akeri, wilayani Arumeru, Arusha.

Habari za kuhamishwa kwa kikao hicho cha siku mbili zimethibitishwa na Mkurugenzi wa Habari na Uenezi wa Chadema, John Mnyika aliyesema kuwa, uamuzi huo umelenga kuwawezesha viongozi wake wakuu wakiongozwa na Mwenyekiti Freeman Mbowe na Katibu Mkuu, Dk. Willibrod Slaa kuwa karibu ili kujumuika na kuifariji familia ya marehemu pamoja na kushiriki kutoa heshima za mwisho kwa Sumari.

Wakati Chadema wakiupa uzito msiba huo, ikiwa ni siku chache tangu iondokewe na mbunge wake shupavu, Regia Mtema aliyekufa katika ajali ya gari Jumamosi iliyopita, Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani

Arusha kimeunda kamati mbili za kuratibu mipango ya mazishi ya marehemu.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Goodluck ole Med-eye, alisema hayo akisema kamati hiyo ina wajumbe saba na kamati ndogo itashughulikia mapambo, usafiri na ujenzi wa kaburi la marehemu huyo na mipango yote inaendelea vizuri.

Aidha alisema kuwa shughuli zote zitafanyika chini ya ushirikiano wa ofisi ya Bunge ambao ndio watakaokuwa mstari wa mbele katika mazishi hayo ya Sumari aliyeacha mke na watoto wanne.

Mwili wa marehemu unatarajiwa kuagwa rasmi jijini Dar es Salaam leo kwa wabunge na wananchi kwenye viwanja vya Karimjee.